# FORM TWO KISWAHILI TOPICAL QUESTIONS

AMOBI SOFT COPY PUBLISHERS

Transparency, Honesty and Accountability Defined

## F2 KISWAHILI TOPICAL QUESTIONS

**Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes**

N/B Marking Schemes are NOT Free of Charge

ONLY Questions Are Free of Charge




0706851439
By Sir Obiero Amos Resources

&

+254706851439
AMOBI SOFT COPY PUBLISHERS
Transparency, Honesty and Accountability Defined



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

# INSHA

## 1.INSHA ZA KIUAMILIFU

1. Kitengo kinachohusika na usalama barabarani kimekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanachama watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha ajali nyingi nchini na kutoa mapendekezo yenu jinsi ya kurekebisha hali hiyo. Andaa ripoti yenu.

2. Umehudhuria mkutano wa vijana kujadili njia za kuboresha maisha ya vijana katika jamii.Andika kumbukumbu za mkutano huo.

3. Umefikishwa hospitalini ukiugua. Andika mahojiano kati yako na daktari

4. Wewe ni Afisa Mkuu wa Polisi wilayani mwenu; Andika kumbukumbu za mkutano wa kamati ya usalama uliofanyika hivi karibuni kuhusu mikakati ya kuimarisha usalama wilayani humo.

5. Wewe ni katibu wa chama cha wakulima cha kiteka: Tayarisha kumbukumbu za mkutano mliofanya hivi majuzi.

6. Andika insha juu ya: Maisha yangu ifikapo mwaka wa 2020.


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

7. Ndugu yako ameshtakiwa kwamba mnamo tarehe 12 Agosti mwaka jana, alipatikana na hatia ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Amekutaja kuwa ulikuwa na yeye wakati huo nyumbani na umeitwa kutoa ushahidi juu ya:

alipokuwa wakati huo

Shughuli zake za kawaida

Historia yake

Maoni yako juu ya kesi hii.

Andika insha kuhusu vile utakavyomtetea mahakamani.

8. Andika insha juu ya methali hii; Mtenda jambo asishe ni kama asiyetenda.

9.Andika insha kuhusu UKIMWI

10. “Hamjambo wanafunzi . Ninamshukuru mwalimu mkuu kunialika kuja ili niwafahamishe kuhusu ukimwi …….” Endeleza hotuba hii mpaka mwisho .

11. Mti ukifa shinale na tanzuze hukauka .

Toa hoja zitakazounga mkono usemi , ‘Katika jamii za kiafrika mwanamke angali anadunishwa’

12. Eleza shida zinazoikumba nchi hii na upendekeze suluhisho zinazoweza kutolewa.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

# 2.INSHA ZA KAWAIDA

1. Kumekuwa na kilio kila uchao. Pendekeza njia mbalimbali za kutokomezea mbali umaskini katika jamii yako. Fahali wawili wapiganapo, nyasi huumia.

2. Andika insha itakayoishia kwa maneno yafuatayo:-

3. ....hapo ndipo nilipoapa kwamba sitawahi kumfungulia mtu yeyote yule mlango usiku.

4. Asifuye mvua imemnyea.Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kisa.

5. Utovu wa nidhamu shuleni umesababishwa na mabadiliko katika sekta ya Elimu. Jadili.

6. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno ...ama kweli dunia ni mti mkavu; ukiuegemea utaanguka. Nilikuja kutambua kwamba ni heri uwe maskini wa mali na tajiri wa fadhili kuliko tajiri wa mali na fukara wa utu.

7. Licha ya kufaulu kiasi, utoaji wa elimu ya bure katika shule za msingi na upili umekumbana na matatizo si haba. Jadili

8. Mchuma janga, hula na wa kwao.


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

9. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya………… moyo ulinidunda nilipoona gari letu likibingiria kuelekea ufuo wa bahari, machozi yakanitoka kwa wingi nikakumbuka yote niliyokuwa nimetenda ulimwenguni, nikayafunga macho yangu.

10. Udongo uwahi/upatilize ungali maji.

11. Kuavya mimba ni uovu usioweza kuvumiliwa , jadili.

12. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya:

.................ndipo nilipogundua kuwa mtu ambaye siku yake imefika hana budi kufa hata
akafanyiwa dawa za aina gani.

# UFAHAMU

1. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho n.k. kwa raia, kuna hatari kubwa kwa


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini.

Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharibu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyi kazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vyaafya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umaa wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, whandisi, mawakili, walimu na mahesibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi.. Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwinginehulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza hudumia jamii.

Ufisadi **umekita mizizi** na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyikazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyikazi wenye biddi hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishaia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimeteuliwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya Kuchunguzavisa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni ya shilingi) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupikea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa wakalipa, au wakilipwa kuwatetea mahakamani wanakwepa jukumu hilo ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**Maswali**

1. Eleza aina **nne** za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma

2. Kulingana na kifungu ulichosoma, ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani?

3. Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi?

4. Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini?

5. Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa

6. Eleza mana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni;

   (a) Majukumu

   (b) Kashfa

   (c) Shamiri

   (d) wakilia ngoa

   (e) Waliohasiriwa

   (f) Kita mizizi



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

2. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea. Wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama. Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka, wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.

Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya uchukuzi na mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vithibiti mwendo vilivyowekwa hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawa peleki magari yao kwa ukaguzi mara kwa mara kama inavyopaswa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hao, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kama vile miraa na bangi, hutumiwa sana na watu hawa, na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini utapata kuwa barabara nchini Kenya haziko katika hali nzuri . Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbi mithili ya machimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame.Kinachohitajika ni serikali kuzifanyia ukarabati ili kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo tayari yamejaaa kupita kiasi. Hili litawasaidia wananchi



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi sana kuliko ile ya kilomita 80 kwa saa iliyokubaliwa.

Inafahamika kuwa maafisa wa uslama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita dhidi ya ufisadi na ajali za barabarni, ni mwananchi mwenyewe ambaye alawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wapelekwe kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na wachukuliwe hatua kali, matatizo haya yataisha.

Lakini kabla kufika hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza ya kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

**<u>Maswali</u>**

1. (a) Mbali na ajali za barabarani, taja, tatizo lingine sugu ambalo linakumba nchi ya Kenya

(b) Ajali za barabarani zinasababishwa na nini?

(c) Mwandishi anapendekeza hatua zipi zichukuliwe na serikali ili suluhisho la kudumu lipatikane?



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(d) Taja hatua ambazo serikali imechukua ili kuimarisha uchukuzi

(e) Ni kitu gani ambacho kinaonyesha kuwa serikali imeshindwa kukabiliana na ajali barabarani?

(f) Eleza maana ya maneno haya:-

(i) Tatizo sugu.
(ii) Vithibiti mwendo.
(iii) Machimbo.
(iv) Ukarabati.
(v) Hongo.
(vi) Kuhamasisha..

3. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Nchini Kenya, pamoja na kuwa mwanamke amepewa hadhi kubwa ikilinganishwa na hapo awali, kumetokea visa vingi vya unyanyasajiwa wanawake. Visa hivi haviwakati wengi maini, bali ni vyombo vya kuwazindua viongozi kuona kwamba hali haijafika kiwango cha kuridhisha. Visa vya ubakaji wa watoto wa kike na wazee, na wakati mwingine baba zao, vimetokea katika miaka ya hivi karibuni. Isitoshe, akina mama wengi wamekuwa wahasiriwa wa mivua ya makonde kutoka kwa waume zao, hata kwa makosa madogo madogo. Hivi majuzi mmoja wa wanawake hawa, ambao maisha kwao ni shairi tu, alichomwa vibaya na mumewe, kisa na maanaamejitia kujua kuwa kuna siku ya wapenzi, yaani Valentine day.


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Mwanamke huyu, baada ya kutoa mashambani kuja kujumuika na mumewe kusherehekea siku ya wapenzi, alipata sherehe za kuchoma moto huku mumewe akilalamika kuingiliwa uhuruwake. Mama huyu bado anauguza majeraha ya mwili na moyo!

Mwanamke aliyesoma na kupewa fursa ya kufanya kazi na ajira ofisini naye amekabiliwa na changamoto nyingi. Huyu lazima atekeleze majukumu yake kama mama, mke na mfayikazi. Wengi wa wanawake wanaofanya kazi mjini hulalamika wanafanya kazi maradufu ya wanaume. Mwanamke kama huyu, kama alivyolalamika mmoja wao ambaye ni afisa wa utawala wa mikoa, huanza siku yake alfajiri na mapema kuitayarishia familia staftahi, kisha kuelekea ofisisni ambapo anakabiliwa na migogoro mingi ya kusuluhisha. Arejeapo nyumbani jioni, hali huwa hiyo hiyo, kutayarisha chajio, kushughulikia kazi za shule za watoto na kuichangamsha familia. Maisha yake huwa hivyo, siku nenda siku rudi. Utashangaa mja huyu atayabeba mangapi?

Hali huwa mbaya zaidi kwa wanawake ambao wameingia siasa. Hawa mikasa yao haihesabiki. Mara watupiwe mabezo ya kila aina na wanasiasa wenzao, mara washutumiwe na kutiwa midomoni na wanajamii kwa kuonekana wakichapa kazi na kuwa na uhusiano wa karibu na wazalendo wenzao wa kiume. Maisha yake hupigwa darubini hata nyakati ambazo hayahitaji kuangazwa.

Mwanamke amekuwa kinyago cha kufanyiwa mzaha. Juzi karibu mbingu zianguke alipojitokeza mwana vitimbi mmoja aliyejitia kufanyia utani yasiyohitaji. Alimwasiri mwanamke kama aliyechangia kukosewa heshima kwake kwa kule kutamani kufanywa hivyo. Ingawa wanawake


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

walimshinikiza mhusika huyu kuomba msamaha, upayukaji wake haupaswi kuchukuliwa kama mzaha. Ni ishara ya hisia ya ndani za watu wengi kuhusu mwanamke; kwamba ingawa wakenya wamejitahidi kupigania haki za wanawake; baadhi yetu bado wana zile fikira za kijadi kuhusu wanawake.

Uchumi wa nchi kamwe hauwezi kuendelea bila kumhusisha kila mtu. Nchini humu, baada ya kutambua haya, mwanamke amepewa nyadhifa mbalimbali katika serikali. Ingawa kuna baadhi ya wanawake waliohusika na kashfa mbalimbali za kifisadi, Kuna wale ambao wametumia nyadhifa zao kuhifadhi nchi. Mmoja wa wanawake amejaribu kwa jino na ukucha kuyalinda mazingira dhidi ya mapapa. Nani asiyekumbuka matusi na mabezo aliyopata mwanamke huyu anayejitoa mhanga kuikinga sehemu Fulani ya burudani dhidi ya kunyakuliwa na wanaostahili? Hakuyajutia yaliyompata. Aliowatisha walijaribu kummeza mzimamzima lakini mwishowe walisalimu amri na kuliacha eneo hilo. Hiki kilikuwa kitendo cha ujasiri na uzalendo mkubwa. Matunda yake yamewafaidi wengi, vijana kwa wazee. Kila mwisho wa wiki huwaona watu wakimiminika kwenye eneo hili kujipumbaza. Hii si fahari kwake tu, bali kwa nchi kwa jumla. Wale waliompinga na kumwita punguani wakati huo wamebaki kuinamisha nyuso tu; bila shaka wamefunzwa mengi.

Wanawake sasa wana haki ya kumiliki mali mathalani shamba. Kutokana na hili tumeshuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa chakula mashambani na kwa hivyo kupunguza njaa na umaskini.

Biashara ndogondogo zinazoendelezwa sokoni na mitaani, kwa kiasi kikubwa, huhusisha wanawake. Biashara hizi huchangia pakubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi kwani hutoa ajira ya kibinafsi kwa maelfu ya


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

watu. Ushuru na leseni zinazokatiwa biashara hizi huongezea serikali pato la ndani.

Mgala muuwe na haki umpe. Ni ukweli kwamba tumekuwa na visa vya hapa na pale vya ukiukaji wa haki za wanawake. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba nchi hii imejitahidi mno kuendelea kumkwamua mwanamke kwayo. Hata mashirika ambayo hapo awali hayakupenda kuwaajiri wanawake, sasa yanawapa nafasi sawa na wanaume. Vyuo vikuu vya kibinafsi vimeanzishwa kuwasajili wanawake. Jijini humu, mna chuo kikuu cha sayansi cha wanawake. Aidha kumeanzishwa kituo (shule) cha kuwasajili wasichana kutoka familia maskini kujiunga na kidato cha kwanza. Wasichana hawa watapata wadhamini kutoka mashrika na watu mbalimbali ili kujiendeleza kimasomo.

Kumheshimu mwanamke ni miongoni mwa haki za kibinadamu ambazo shart zitekelezwe. Hata hivyo, wanawake wakumbuke kwamba hata wanapopuliza siwa kuhusu pupewa haki, lazima wao pia wawajibike. Wao ndio walimu wa kwanza wa wanao; ikiwa basi wataonekana kwenye vyombo vya habari wakining’inia juu ya magari ya wachunga magereza kwa kuzitafutia pesa za mayatima maumizi bora, watakuwa wanapotosha watoto wao. Wawe watu wa vitendo zaidi ya upayukaji.

## Maswali

a) Kwa mujibu wa taarifa, ni mambo yapi yanayoonyesha ukiukaji wa haki za wanawake



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

b) Fafanua jinsi mwanamke aliyesoma huteseka maradufu zaidi ya mwanamme

c) Ni faida gani ambazo zimepatikana kutokana na wanawake kupigania haki zao?

d) Hatimaye wanawake wanahimizwa kufanya nini?

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotumiwa katika nakala

Kinyago…

Mabezo

f) Andika mfano wa mbalagha na uhuishi uliotumiwa katika makala haya

i) Mbalagha…………

ii) Uhuishi…………

4. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:-***

Uundaji wa istilahi – hasa za lugha ya Kiswahili ni shughuli nyeti na nzito hivi

kwamba, haipaswi kupapiwa na mtu yeyote. Hii ni shughuli inayohitaji umakinifu zaidi kwa wanaoshiriki katika mchakato wa uundaji istilahi za kutufaa katika mawasiliano na kukuza Kiswahili kwa jumla. Ufanisi wa watu binafsi, vyombo vya habari kama vile Shirika  la Habari la Kenya (KBC),



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Taifa Leo na mashirika mengineyo katika ukuzaji wa lugha hutegemea mno sera na utayarishaji wa serikali katika kugharamia shughuli hii. Aidha, shughuli za kukuza lugha hukwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha pamoja na sera maalum ya serikali kuhusu lugha.

Hata hivyo, katika kuyakwepa matatizo haya, pamekuwepo na hatua za kimataifa za kujaribu kusawazisha shughuli ya uundaji wa maneno. Hatua hii ilichochea kubuniwa kwa shirikisho la kimataifa la vyama vya usanifishaji istilahi mnamo 1936. Lengo la kitengo hiki lilikuwa ni kufafanua msingi madhubuti ya uundaji wa istilahi duniani. Kwa hakika, shirikisho hilo limesaidia mno katika kuweka misingi ya shughuli za ukuzaji wa istilahi. Misingi hiyo ni ya jumla na haihusu taaluma yoyote mahususi. Katika makala hii, tunapiga darubini baadhi ya misingi hiyo pamoja na mapendekezo yake.

Mosi, uundaji istilahi unafaa uanzie kwenye dhana na wala sio neno. Hii ina maana kwamba, kwanza pawepo na dhana au hali ambayo inahitaji itafutiwe neno au istilahi ya kuielezea. Inasikitisha sana kwamba pana wataalamu ambao wanaukaidi au kuukiuka msingi huu. Wanataaluma hawa hufanya mambo kinyume kwa kujibunia maneno yao na kuyahifadhi kwenye mikoba yao – halafu wakasubiri dhana izuke ndiposa waipachike istilahi yao. Pili, dhana zinabuniwa au kutolea istilahi au maneo ni muhimu zielezwe kwa ukamilifu na uwazi. Istilahi zinazoundwa zinafaa ziwe fupi iwezekanavyo na ziwe na uwezo wa kuelezea dhana kwa njia inayoeleweka bila utata. Tatu, maneno yanayoundwa sharti yawe na uhusiano wa aina fulani na dhana zinazowakilishwa na maneno hayo.

Uhusiano huo unaweza kuwa ama ni wa kimaumbile au wa kiutendaji. kwa mfano, Mzee Sheikh Nanhany wa Mombasa alipobuni istilahi ‘uka’ kwa



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

maana ya 'ray'. Neno hili latokana na kupambauka au (kupambazuka kwa lafudhi ya kiamu. Neno 'image' ni jazanda kwa Kiswahili. 'Mirage' kwa Kiswahili ni 'mangati' (kutoka kwa mang'aanti) – yaani kung'aa kwa nchi. Mtaalamu mwingine aliyewazia uendajikazi wa kifaa na kubuni istilahi inayokubalika mpaka sasa ni Prof. Rocha Chimerah ambaye alibuni istilahi 'tarakilishi'. Pengine Prof. Chimerah alifikiria kazi ni kifaa husika na kuunda neno la Kiswahili linaloakisi kazi hiyo. Tunajua kwamba kompyuta hufanya kazi inayohusu tarakimu kwa haraka kama umeme. Labda Chimerah ameegemea sifa hii kuibuka na istilahi hii.

Maneno mengine ambayo yamebuniwa kufuatana na msingi huu ni ya Mzee Nabhany-mathalan 'barua pepe' (e-mail), na wavuti (website). Tukiegemea maumbile, neno 'kifaru' lina maana ya vita ilihali tuna zana ya vita iliyopewa jina hilo kwa sababu ya labda kuwa na maumbile sawa na kifarumnyama. Nne, istilahi zinaweza kukopwa kutoka lugha nyingine. Yamkini hakuna lugha hata moja ulimwenguni-zikiwemo lugha duniani kama vile kiingereza zinazoweza kujitosheleza. Takriban asilimia 80 ya maneno katika kiingereza ni ya kukopwa. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inapokopa, hali hiyo haipaswi kuchukuliwa kuwa ni lugha dhaifu.

Hata hivyo, istilahi zinazokopwa zi-nafaa zichukuliwe zilivyo katika umbo lao asili. Umbo hili linaweza kufanyiwa marekebisho machache tu, kulingana na sarufi na matumizi ya lugha kopaji. Mifano ya istilahi kama hizi ni 'televisheni' (television), kopmpyuta (computer), kioski (kutokana na jina 'kiosk' la Kijerumani) na redio (radio), Tano, pale istilahi haiwezi kukopwa, lugha husika ijaribu kubuni msamiati ufaao, kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba, lugha inastawi. Lakini tahadhari inapaswa kuchukuliwa hivi


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

kwamba, Kiswahili kisikope maneno kiasi cha kupoteza upekee wake. Mwisho, uundaji wa istilahi uzingatie mofolojia ya kawaida ya lugha. Istilahi zinazoundwa kwa kuzingatia mofolojia huwa rahisi kuiua maneno yenye uhusiano wa istilahi asili kwa njia ya mnyambuliko.

**Maswali**

(i) Taja mambo ambayo huchnagia ukuaji na ufanisi wa jumla wa lugha ya Kiswahili

(ii) "Lugha ya Kiswahili ni dhaifu na isiyotosheleza" Je, mwandishi wa makala haya ana msimamo upi kuhusu kauli hii?

(iii) Tahadhari zipi zinazofaa kuchukuliwa kabla ya kukopa istilahi kutoka lugha zingine?

(iv) Yape makala haya anwani mwafaka

(v) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

(a) Dhana-

(b) Takribani –

(c) Istilahi –

.

(d) Mofolojia –...



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

## 5. UFAHAMU

1. ***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:***

Miaka michache iliyopita, kila aliyekuwa amesoma alikuwa na bahati ya kupata kazi katika ofisi za humu nchini. Wote waliofika darasa la saba au pengine kidato cha pili na zaidi wale waliofuzu mtihani wa kidato cha nne, walinyakuliwa juu kwa juu na wizara mbalimbali za serikali au pengine waliandikwa kazi na makampuni. Kwa vile kila moja wao alipata kazi ya kuajiriwa, hakuna aliyejishughulisha na kazi za mtu binafsi kama useremala, uashi, ukulima, uvuvi na kadhalika- kazi kama hizo ziliachiwa wale tu ambao hawakupata fursa ya kuenda shule.

Siku hizi mambo yamebadilika. Licha ya kuwa na elimu ya darasa la saba au kidato cha pili na pengine cha nne, hata wale wenye shahada za vyuo vikuu nao pia wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga; na wale ambao bado hawajakata shauri kama hili, wako barabarani wakipiga lami.

Wakoloni walifanya kosa moja kubwa sana ambalo tumeligundua tu baada ya kunyakua uhuru wetu. Kosa lenyewe ni lile la kuwafanya wananchi waliopata elimu wasipende kushika kazi zinazochafua mikono.Walijua tu kwamba mashamba yao na hata mitambo yao ingalifilisiwa na ile ya waafrika; kwa hivyo ingaliwabidi hata wao waje wawatumikie wenyeji. Ndipo walipokata shauri kutowaamsha waliolala ili wasije wakalala wao.

Katika karne hii, wataalamu wameshawishika kuitumia elimu yao kufanya kazi za mashamba, ujenzi na ufundi wa mitambo. Ijapokuwa baada ya kazi kama hizo mikono huwa imejaa tope au masizi, pato lake ni kubwa ajabu. Jambo la kuvutia


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

zaidi katika makazi kama haya ni kwamba mwananchi huwa ni ‘bwana’ mwenyewe, hujitegemea mwenyewe bila kochokocho.

Kila moja wetu yuaelewa kinaganaga kwamba kazi kama ya ukulima huleta donge kubwa zaidi ya kazi zote; kwani kila mfanyikazi humwelekea mkulima baada ya kumaliza kazi yake. Mkulima naye hutoa jasho jingi wakati wa kulima shamba. Baadaye atapekua magugu na visiki aviweke katika matita ili aviteketeze moto. Baada ya muda kidogo atapanda na angoje hadi mbengu zake ziaanze kuchipuza. Mara maua huchanua na mazao kujionyesha. Baada ya kuvuna, kazi yake kubwa huwa ni kuanika na kuanua nafaka zake. Wakati huo, mazao yake huwa yatanga, mara yuapanga mara yuapangua mipango juu ya uuzaji. Mazao yafikapo nyumbani, pengine mkulima huipamba nyumba yake na akawaita marafiki zake ili awakirimu kwa vyakula na vinywaji. Karamu ikiisha hana budi kupambua mapambo yote. Huyoo, aenda kuuza bidhaa zake; akirudi yuakaa raha mstarehe akila na kuburudika pamoja na familia yake. Je kuna kazi yenye raha zaidi ya ukulima?

Watu wengi hufikiria maana ya neno ‘kulima' ni kushika jembe tu. Hiyo si kweli kwani kuna ukulima namna nyingi, kama vile ufugaji wa ng’ombe, mbuzi au kuku. Hata ufugaji wa samaki au utunzaji wa nyuki pia waweza kuitwa ukulima. Dhamira ya taifa letu changa ni kuwapatia mwangaza wananchi wake waliomo mashuleni, kwamba wangojewa kwa hamu wajiunge na wenzao katika kulijenga taifa lenye nguvu, ili katika kujisaidia wenyewe pia waongeze pishi katika kulipa taifa maongozi mema yasiyokinai kazi zilizokuwa zikiitwa ‘chafu' lakini ambazo ndizo hasa kiini cha maendeleo na kujitegemea.

a) Kulingana na habari uliyosoma, ni mambo gani hasa yaliyochangia kupuuzwa kwa kazi za mtu binafsi? (alama 3)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

b) Wakoloni walikuwa na lengo gani kwa kufanya waafrika waliosoma kuchukia kazi za mikono? (alama 2)

c)Unafikiri mwandishi wa taarifa hii alikuwa na dhamira gani kwa wasomaji wake? (alama 2)

d) ..'Wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga' Mwandishi anamaanisha nini katika kauli hii? (alama2)

e) Kwa nini wasomaji wa kisasa wameanza kufanya kazi ya ukulima? (alama 3)

f) Eleza maana ya semi hizi kama zilivyotumiwa katika taarifa: (alama 4)

i) Kata shauri

ii) Kuwa bwana

g) Mwandishi ametumia maneno yenye maana ya kinyume kwa mfano 'panga na pangua'; yataje maneno mengine mawili yaliyotajwa na vinyume vyao huku ukieleza maana ya kila moja ya maneno hayo. (alama 4)

**6.UFAHAMU**

Kama kawaida yake , Faki alifika hospitali saa kumi na mbili asubuhi . Kawaida hii haikuanza zamani sana kwa hakika : Imeanza karibuni tu , toka kitoto chao chanajike kilipolazwa hospitali kwa <u>tumbo la kuendesha</u>.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Masika mama-mtu ikambidi akikimbie kitanda cha kinyumba kulalia kitanda cha hospitali karibu na mwanawe . Na Faki kwa upande wake ikamlazimu kutamba na jua na mvua kuizumbua riziki angalau ya kupeleka mkono kinywani.- angalau riziki hiyo! Na alipoipata riziki ya mchana kutwa alijifunga kibwebwe kuingia jikoni kuitayarisha ilike , kisha kudapia baiskeli yake au mwanapata kama watu wengine wanavyoita kuelekea hospitali kumpelekea mama mtoto aghalabu muhogo wa kupwaza na chai ya mkandaa; na kile kitoto chao , maziwa na uji

Asubuhi kila siku ilimbidi atoke mapema , kisha ashike njia kuelekea kibaruani .

Naam , kama kawaida yake , leo aliuwacha mparapata wake nje chini ya ngazi pale hospitali, akatoa mkoba wenye uji na maziwa ya mtoto pamoja na muhogo wa kupwaza na chai ya mkandaa ya mama - mtoto ,kwenye lile boksi kubwa analolifunga kibaoni nyuma ya baiskeli yake . Huyo Faki akawa anapanda ngazi taratibu kuelekea wadi ya watoto kumwuona mwele na muuguzi wake

Lakini leo , kabla hajamaliza kuipanda ngazi , alisikia ukwenzi wa mwanamke ambao ulimtuturisha moyo . Asingaliweza kuipotea sauti ya mwanamke huyo ingawaje ilitoka kwa ukwenzi . Bila shaka ilikuwa sauti ya Masika mkewe . Na sasa ukwenzi huo uwe wa nini ? Uwe wa nini enh, isipokuwa ……….

Alitimka, akazipanda ngazi kwa vidato vitatu vitatu. Macho yakamtoka na moyo ukamhaha . Joto la ghafla likamjia. Na hofu ikamjaa. Huyo kufumba na kufumbua, alijkuta katika mbele ya Masika mkewe aliyekuwa kashikiliwa



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

vyema na wauguzi ; wengine kulia na wengine kushoto huku akiwawa na kupiga makambi na mayowe .

“Nini ?” Alibwata Faki pale alipokuwa kasimama kama shujaa aliyechomwa sime na kuyasikiliza maumivu. “ Mwanangu …….” Alipayukwa Masika, “ maskini damu yangu … mume wangu ewe mwenzangu…… nguvu zetu, jasho letu, mtoto …….aaaa mama! Uchungu wa mwana unauma! Tumbo linanikeketa !” Aliendelea kulalama Masika.

Lugha hiyo ilitosha kujibu swala la Faki lililomwenda akilini. Kila kitu kilikuwa wazi. Faki sasa alikwisha maizi nini kimetokea. Hima alipiga goti chini kufikia kimwili kilichozongwa shiti jeupe na kulazwa kigodononi sakafuni. Huku mwili mzima ukitetema, taratibu alinyoosha mikono kukiteka hicho kijimwili kisha aliinuka na kwenda nacho kwa mkewe.

“ Mume wangu, haaikuwa riziki yetu …..” aliendelea kulia Masika

“Nyamaza Masika”, alitamka Faki kwa upole huku akijaribu kuyazuia machozi yaliyokuwa njiani . “ Kila liandikwalo halina budi kuwa, lazima ….”

alishindwa kuyamaliza aliyotaka kuendelea kuyasema .

**Maswali.**

(a) Eleza kwa nini Faki alikuwa akienda hospitali kila siku *(alama 2)*



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(b) Taja jina lingine lililotumiwa katika taarifa kurejelea baiskeli *(alama 1)*

c) Kwa nini Faki alilazimika kutafuta kibarua kila asubuhi *(alama 3 )*

(d) Eleza sababu iliyomfanya Masika kupigwa ukwenzi *(alama 2)*

(e) Unadhani mwandishi ana maana gani anaposema, "……ilitosha kujibu swala la Faki lililomwenda akilini kila kitu kilikuwa wazi" (alama 3)

(f) Fafanua maana ya, " mume wangu haikuwa riziki yetu ……" *(alama 3)*

Taja maneno yoyote mawili kutoka kwa taarifa ambayo yamefanyiwa utohozi kutoka lugha ya kiingereza *(alama 2)*

(h) Eleza maana ya ; *(alama 4)*

Alijifunga kibwebwe

Machozi yaliyokuwa njiani

7.

**UFAHAMU**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**

Msemo "Ya kale hayako" unatukuzwa sana na vijana na hata wazee ambao wanathamini usasa. Msemo huu umetishia kuumeza na kuutema utamaduni wa Mwafrika. Utamsikia kijana akiambiwa na mzazi wake, "Jamani itabidi ujifunze lugha yako ya mama, hivi hatuwezi kuwasiliana na mababu zako kijijini". Naye kijana huyu hujibu, huku macho kayatunga kwenye runinga, kidhibiti mbali mkononi. "Hayo ni yako. Lugha inahitajika kutumiwa pale mtu anapoishi. Mimi kijijini humo nitaishi lini? Na huyu babu, si anajua Kiingereza?"



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Huyu ni mfano mmoja tu unaoonyesha mabadiliko ambayo yamezikumba jamii zetu. Watoto na hata watu wa umri wa makamo wamerithi desturi mchafukoge ambazo hazijulikani kama ni za Kiafrika au Kizungu. Mitindo ya mavazi ya kushangaza imezuka. Kuna wale wanaopendelea kutembea mabega wazi. Hawa huvaa vizibau vilivyoning'inizwa kwenye fito za nyuzi. Kuna baadhi ambao huvaa suruali ndefu ambazo zimening'inia kiasi cha kuvifanya viuno kuwa kwenye miundi. Huu nao ni usasa ati. Unapouliza unazomewa na kuambiwa umechelewa kutambua hii ni karne ya ishirini na ngapi.

Tofauti za umri zimeanza kuwa finyu mno siku hizi. Si bura kumpata kijana akimpita mzee kama kwamba hajamwona. Anangoja mzee amsalimu yeye. Vijana wengine hudiriki kujibizana na wazee wao kama kwamba ni wa rika moja. Hawawapi wazee fursa ya kuzungumza, badala yake huwakata kauli kila mara wanapozungumza na kuwaudhi. Anapoulizwa kwa nini anamjibu vibaya mzee huyo, anasema nyakati za 'kuhubiriwa' bila kuuliza maswali zimepita na kuzikwa.

Teknolojia mpya imewapunguzia udhia baadhi ya vijana ambao hawapendi kufanya kazi. Katika baadhi ya familia, utapata kwamba kuna mashine za kufulia nguo na kupangusia sakafu. Vijana wengi wanaoinuka hawawezi hata kujifulia nguo. Wale ambao kwao hakuna mashine, wana vijakazi ambao huwafanyia kila kitu. Lao ni kulala tu na kusoma. Mafunzo ya kazi ambayo vijana walipata siku za mababu yameanza kuzikwa kwenye kaburi la sahau. Hata katika familia ambazo utapata wazazi wana ari ya kuwafunza wanao umuhimu wa kutenda kazi za nyumbani, utapata kwamba watoto wenyewe hawazipendi kazi hizi. Wanahiari kucheza michezo ya kompyuta na kutazama kupigana mierekani na masumbwi katika


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

runinga. Si ajabu kwamba wengi wa vijana wanakua wakidhani njia ya kutatua migogoro ni kupitia kwa makonde migoto vichwani.

Suala unasaba lilikuwa na umuhimu mkubwa katika siku za kisogoni. Neno ndugu lilikuwa na maana pana katika jamii ya Mwafrika. Watoto wa ami, mjomba na shangazi walihifadhiana na kulindana kama ndugu. Siku hizi neno ndugu limejikita tu katika uhusiano wa karibu tu; mtoto wa mama au baba yako. Vijana wengi hawajui hata mabinamu zao. Jambo hii limewafanya wengine kuoa watu wa ukoo wao bila kujua. Baadhi ya vijana wamezaliwa na kukulia mijini, hawana wakati wa kutangamana na jamaa zao vijijini. Kwa hivyo, hata inapofika wakati wa kuoa, hao hukutana na wachumba wao mijini.

Ingawa tunapasa kutambua kuwa wakati umebadilika, ni vyema kuwajibika. Hata pale tunapoiga mitindo ya kisasa kama vile ya mavazi, tuige kwa tahadhari. Mavazi tunayovaa yasikinzane na maadili ya jamii zetu. Elimu ya kisasa isiwe kisingizio cha kusahau kitovu chetu. Tukumbuke methali isemayo "Usiache mbachao kwa mswala upitao".

(a) Mwandishi amedhamiria kichwa mwafaka cha taarifa hii kuwa ya kale hayako. Eleza.

(alama 2)

(b) Tofauti za umri zimeanza kuwa finyu mno siku hizi. Fafanua kauli hii. (alama 2)

(c ) Mabadiliko yaliyokithiri katika jamii ni kutokana na vijana wasiowajibika. Toa ithibati. (alama 5)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(d) Eleza chanzo cha mabadiliko ya vijana kulingana na taarifa. (alama 4)

(e) Eleza matumizi ya methali usiache mbachao kwa mswala upitao kulingana na taarifa. (alama 2)

**8.UFAHAMU**

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>***

Siku moja , mtu ambaye alijulikana kwa jina la Moto , alikuwa Ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni, ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Kupitia mbuyuni, iliwabidi kwanza wapitie pale mtegoni. Lakini kwa kuwa kwa siku hii ya leo wakati wao wa kunywa maji ulikuwa bado kuwadia, naye Moto, badala ya kurudi ili aje baadaye, akaonelea heri angojee hapo.

Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi na kwa muda mrefu sana. Na ingawaje alifurahia nyama yao laini, ni kuwachuna ndiko alikokuzira. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya vifaa butu vya mawe ya kuchonga alivyokuwa akitumia. Kwa sababu hii basi, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia, alikuwa akiwala wabichi. Ili kujipa kazi akisubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo ungekuwa wa namna gani. Nyakati hizo, shanga zilikuwa bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilivyokuwapo, navyo ndivyo vilivyokuwa mali ghafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga, Moto akakata vijiti viwili. Kikubwa akakiita 'mama' na kidogo, 'baba'. Dhamira yake ilikuwa kumtengenezea mkewe



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

ushanga na tembe zikiwa za mti. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekejea tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote, Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi, halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa muaa ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha, na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuwa tsanzala ambayo ilienea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe! Kutoka kwa upande wa mtegoni, kukaja harufu nzuri ya kunukia. Alifuata na alipofika, akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Kwa hivyo, hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma sembuse cha kupikwa!

Ni harufu ya kuiva ya kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona ndivyo vilimtia ujasiri. Naye kwa hatua za woga, akanyatanyata akanyakua kinofu na kukionja. Si utamu huo aliousikia! Sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki, akamfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake. Pamoja na kulungu, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita "wimbombo" na kijiti baba, " ulindi"...


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Ilikuwa alfajiri asubuhi watu waliposhitukia "tatata" za kualika kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa Moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho. Kiliwavutia zaidi kwani walivyozidi kulisongelea, ndivyo ile baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Lakini walipumbazika zaidi walipoona - nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

Macho yake yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa sababu ya moshi; lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha. Wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bambuazi, wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo ndipo waliposikia sauti ikinena: "Mimi ndimo Mooотоо...; naivisha na kuunguza, natokeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake nimpe huu uwezo wangu..."

Ili kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi zilizowafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi, akaendelea kuwatia woga kwa kusema, "Hizi ndizo nguvu za Moootoo... mimi ndimi Moootoo...nijieni niwageuzie maisha yenu..."

Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akawagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo aliwaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo, badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao, kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita "Moto".

Punde si punde, watu wakawa wamezoea moto na wengi wakawa wanakuja kwake tu. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo, akaweka masharti: moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo "moto mpya" ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuuiba ama kuuficha, basi asije kulia kwake baadaye, akawaeleza.

Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa - na punde si punde, za utukufu pia! Sasa watu wakawa, bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia:

“Ili kuulinda huu Moto Mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu."

" Tutakugawia chakula chetu ili uzidi kuuchunga huo Moto Mtakatifu ili usife," wakamkatiza.

Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto".

**Maswali**

Ipe makala uliyoisoma anwani mwafaka (alama 1)

Moto alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu kwa sababu gani? (alama 2)

Ala za pekee za wakati huo zilikuwa zipi**?** (alama 2)

Uvumbuzi wa Moto ulikuwa na athari zipi katika maisha ya jamii? (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kwa kutotaka Moto uenee hivi hivi tu, Bwana Moto aliuwekea masharti. Taja mawili (alama 2)

Moto na Aila yake walifaidikaje baada ya ufumbuzi huu? (alama 2)

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa.(alama 4)

Kioja

Alikokuzira

meza kichaka

wimbombo

**9.UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti kabisa na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake-kuu.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Yeye hataraj ii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia mumewe watoto, na daima dawamu kuwa 'mwendani wa vijungu jikoni' akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamananamwanamume. Akanyagapo mume, nave papo huutia wayo wake.

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kuj ifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, historiajiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutakakufanyakaziyakibega,akazifanya.

Akatakakuwamwalimu,akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamme siku

hizi.

Mwanamke wa kisasa hateswi akafyata ulimi. Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kuhifadhi yaliyopitwa na wakati.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha ukatani.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katikajambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanamume wa 'kisasa', ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume. hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwambamamabadiliko haya sio mithili yakiwingu kipitacho, bali ni ya aushi.

Maswali:

a) Msemo 'mwendani wa vijungujiko' unadhihirishahali gani ya mwanamke katikajamii? (alama 2)

b) Jamii imemfanya mwanamke kuwa hayawaniwamizigo. Fafanua (alama 1)

c) Eleza maana ya'akanyagapo mume, naye papo huutia wayo wake." (alama 2)

d) Zungumzia maswala ya ndoa na elimu huku ukilinganisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa (alama 4)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

e) Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (alama2)

f) Taja mifano minne ya 'mawazo yakihafidhina'. (alama 4)

g) Eleza maana ya:

i) Akafyata ulimi ii) Ukatani

iii) Taasubi za kiume.

iv) Aushi (alama4)

**10.UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Nchi nyingi za ulimwengu unaoendelea, au ule uliokuwa ukiitwa ulimwengu wa tatu zimegawika sehemu mbili mbili. Sehemu hizi zinazidi kutoshabihiana kila uchao. Zinatengana kiasi cha kukaribia kupigiwa mfano wa masafa ya ardhi na mbingu. Sehemu zenyewe ni mij ini na mashambani. Sehemu hizi, hasa ukizitia katika mizani ya hali na jinsi za watu za maisha, zimetofautiana mno. Kiasi cha tofauti hizi ni kikubwa hadi kuonekana kama kwamba hazinauhusiano kamwe, mithili ya nchi mbili tofauti. Hebu sasa tuzingatie yale yanayozifanya sehemu hizi



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

kutokosa kufanana. Hapa tutawajibika kuzizingatia tofauti zilizo bayana baina ya watu wa shamba na wa mij ini, hasa kufungamana na jinsi wanavyoyaendesha maisha yao.

Jambo lililo wazi ni kwamba watu wa mashambani hawajapiga hatua ya maana kuhusu jinsi wanavyotakikana kuishi katika karne ya ishirini. watu hawa bado wanaishi kama walivyoishi mababu zao. Hawdhisi halahala ya jambo lolote. Matengemeo yao ni shamba; usubiriwe msimu mzuri wa mvua, watu walime, Mungu akineemeshe kilimo, wavune mavuno mema, basi. Wakisha yatia maghalani wachukue kidogo kidogo na kiitayarisha kwa chakula. Chakula kikiwa tayari, wale, walale, siku nyingine warudie mkondo uo huo wa kuendesha rnaisha yao.

Watu hawa maisha yao yamepangika mikondo mitatu tu: kuzaliwa, kuoa na kuolewa, na kufa. Zaidi ya mikondo hii, maisha ya viumbe hawa hayana mabadiliko makubwa. Mabadiliko hayapendelewi sana huko mashambani. Huko, wanaume ni mabwana, wanawake ni mfano wa vij akazi na watoto hawana tofauti kubwa na watwana. Mwanamume akikohoa, mkewe akimbilie kulikokoholewa/an watoto wattetemeke.
Wanawake wa shamba na watoto hawana haki hata ya kunena, wala hawajui haki ni nini.

Kwa upande mwingine, mijini kuna viwanda, kuna m|ijumba, kuna magari na kuna vyombo vingi sana vya maendeleo ya kjsiku hizi. Watu wa mijini ni watu wa ulimwengu kote, wala si watu wa mji mmoja tu. Watu wa mji wowote


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

ulimwenguni huweza kuwasiliana na wenzao wa miji mingine kpkote kule ulimwenguni, hata papo kwa papo kwa njia ya runinga. Pia, kwa watu wa mjini, kuona Kiumbe kidogo kabisa kisicho weza kuonekana kwa macho si ibura hata. Kiumbe cha namna hiyo huonekana kupitia mangala. Na kwa wale walio ondokea kuwa wanajimu wa kisasa, kuziona sayari na thurea zilizoko mbali sana nasi kupitia nangala nijambo la kawaida sana.

Watu wa mjini huwa na mabadiliko mengi sana katika maisha yao, wala sio mikondo aina tatu tu. Kwa mfano, wanawake wa mijini hawakubali tena kuonewa na wanaume. Wanajua vyema sana maslohi yao na wameiweka menke yao mbele; yaani mahali pao katika jamii, wakiwa wao ni wanawake. Hawaoni tofauti baina ya menke yao na ile ya wanaume. Kwa sababu hiyo wameondokea kupigania haki sawa na wanaume bila k ulegeza kamba. Huku kupambana kimaisha kama wapambanavyo wanaume kumewafanya wanawake wengi mij ini kutowaogopa tena wanaume nakufanikiwa kufanya kazi za kusifika kama vile uwakili, udaktari, uhandisi, urubani na i lyinginezo zilizokuwa zikifanywa na wanaume tu. Wanawake wengine hata ni maprofesa! Kweli watu wa mijini wameendelea.

a) Toa maelezo kuhusu tofuati zinazosemekana ni bayana baina ya maisha ya watu wa shamba na yale ya watu wa mijini (alama2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

b) Rejelea "Mungu" katika aya ya tatu na neno "viumbe" katika aya ya nne. Bainisha uhusiano uliopo baina ya maneno haya mawili, hasa ukizingatia jinsi yalivyotumiwa katika habari. Je, matumizi haya yanakupa hisia gani? '(alama 4)

c) Unadhani mwandishi ana maana gani anaposema ya kwamba huko mashambani

"wanawake ni mfano wa vij akazi na watoto hawana tofauti kubwa na watwana?" (alama 4)

d) Orodhesha vifaa vyovyote vitano vilivyotaj wa katika taarifa hii, kisha ueleze umuhimu wa kila kimoja wapo.

e) "Watu wa mijini ni watu wa ulimwengu kote." Hapa mwandishi anamaanisha nini? (alama 2)

f) i) Ni nini maana ya neno menke? (alama 1)

ii) Mwandishi anamaliza taarifa yake kwa kusema "Kweli watu wa mijini wameendelea." Kwa muhtasari, ni tabia gain za wanamiji zilizomfanya kukiri hivyo. (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**11.UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswaliyanayofuata.***

Katika falme ya Pate ya enzi za kale, kulikuwa na binti Sultani aliyeitwa Mwanakishwira. Alipopata umri wa miaka kumi na minne tu, Mwanakishwira alikuwa tayari ni mrefu na mkubwa, na alionekana kuwa msichana mzima mwenye umri wa miaka kumi na minane. Alikuwa nadhifu na mzuri sana wa sura, kiasi cha kubandikwa lakabu ya malaika. Alipendeza sana macho <u>fauka ya kuwa</u> alikuwa na akili nyingi mno. Katika umri huo, alikuwa amemaliza masomo yake yote katika madrasa iliyokuwa hapo, na aliweza kuikariri Kurani yote bila kigezigezi. Babake, Mfalme, aliuma vidole akilia ngoa kuwa mtoto mwenye akili hiyo ni mke wala sic mume. Aliwaza ya kuwa kama angekuwa mvulana, angempeleka zutafindaki ya Al-zhar huko Misri kuendelea na masomo ya juu katika chuo hicho kisifika.

Wakati Mfalme akiuma vidole kuhusu jinsia ya mtoto wake, wanaume wengi hapo mjini walikuwa wakimeza mate. Mtu aliyemezewa mate alikuwa ni yeye huyo Mwanakishwira. Walimmezea mate kwa sababu kila mmoja wao alitaka kumwoa awe mkewe. Kumwoa Mwanakishwira kulikuwa na manufaa ya kupata mke mwenye uzuri wa shani, kama nyota, na aidha kuwa Mfalme baada ya mweye kukikalia kuaga dunja, sababu yeye hakuwa na mrithi mwingine.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Basi ikawa ni kila mtu kujipendekeza kwamfalme, kwa vile alikuwa anasumbuliwa sana, na wakati huo huo aliogopa kuwa asipomwoza mapema binti yake huenda akaharibika, akaamua kuruhusu wachuma wamchumbie.

Uamuzi huu ulimshtua sana Mwanakishwira, Mshtuko alioupata ulimtia ugonjwa na kumdhoofisha kabisa. Akadhoofika hadi Mfalme akaingiwa na hofa ya kuwa mtoto wake atakufa. Akaamua kumwuliza kinachomdhoofisha. Mwanakishwira akasema kimdhoofishacho ni mwezi. Akipata mwezi, na nafuu pia ataipata.

Kusikia hivyo, Mfalme akatokwa na kijasho chembamba. Akafikiria kwamba labda mtoto wake amemalizwa kabisa na uwele, na sasa yuaweweseka tu, wala hana akili razini ya kutambua na kupanga mambo.

Hata hivyo hakuvunjikamoyo kabisa. Akaamua kupata tafsiri ya kitendawili hicho kutoka kwa waheshimiwa wake hapo mjini ambao wote walitaka kumwoa Mwanakishwira.

Kwanza akamwendea Waziri Mkuu akamwuliza tafsiri ya mwezi autakao binti yake. Waziri akasema mwezi utakikanao ni wa dhahabu. Alipoambiwa hivyo motto akazidi kudhoofu. Mfalme akakasirika sana. Akawaendea wakwasi wengine kama vile Kadhi, Mnajimu na kadhalika. Hawa wote wakamzidisha ugonjwa binti Mfalme kwa sababu jawabu walizotoa ni kuwa mgonjwa alihitaji mwezi wa almasi, fedha, na hata hatua!

Mwisho kabisa, Mfalme akamwendea mvulana aliyekuwa mchungaji. Huyu akamwahidi Mfalme kwamba aulizwe mgonjwa aseme mwenyewe aina ya mwezi


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

autakao. Jawabu hili halikumfurahisha Mfalme, japo alienda kamwuliza binti yake, kama alivyoambiwa. Alipoulizwa, Mwanakishwira akasema mwezi autakao ni kishaufu kilicho na umbo la mwezi mchanga kilichotengenezwa kwa chuma. Mfalme alishangaa sana. Hata hivyo akamfulia kishaufu alichokitaka mgonjwa. Alipokivaa, Mwanakishwira akapata nafuu mara moja na akaendelea na nafuu hiyo hadi akapona kabisa.

Kuona hivyo, Mfalme akawateremsha vyeo wakwasi wote humo mjini, na kuteua wengine mahali pao. Kwa upande mwingine, mchungaji akaozwa binti Mfalme na kupewa madaraka ya Waziri Mkuu. Hatimaye, Mfalme alipoaga dunia, mchangaji akawa

Mfalme, na Mwanakishwira akawa Malkia.

**Maswali**

a) Zungumzia swala la menke (yaani mahali pa mwanamke au mwanamume katika jarnii katika falme ya pate ya enzi hiyo. (alama5)

b) i) Kwa nini Mfalme aliwauliza wakwasi kwanza tafsiri ya kitendawili?(alama 2) ii) Kwa nini mfalme alishangazwa najawabu la binti yake? (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

c) "Akili ni nywele, kila mtu ana zake." Dhihirisha jinsi methali hii inavyobainika katika hadithi hii. (alama 4)

d) Ni nini maoni yako kuhusu mwanamume aliyemwoa Mwanaki shwira na kwa nini alikubali kuolewa nahuyo? .

e) Eleza maana ya maneno na tamathali za semi ziftiatazo (alama 4)

i) fauka ya kuwa ii) akiliangoa iii) uzuri wa shani iv) akamwaidhi

**12.UFAHAMU**

***Soma makala yafu&lhyo kisha ujibu maswali***

Kati ya viumbe wote waishio ulimwenguni, hakuna kiumbe aliyepevuka kama binadamu. Kiumbe huyu amewapiku wale wengine kwa njia nyingi, hata kuweza kuwatawala na kuwapangia maisha yao. Binadamu amekirimiwa uwezo wa kuyatawala mazingira nakukabidhiwa mazingira hayo. Hekima hii humwezesha kusitiri kizazi chake.

Aidha ametunukiwa uwezo mkubwa kuivinjari sayari hii yetu katika ilhamu yake ya kutaka kuvumbua ‘siri’ za maumbile, amejasiri hata kuzitalii sayari zingine



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

nje ya uso wa ulimwengu huu. Si ajabukwamba iwapo wanyama wengine wangepewa urazini wa kuongea kama yeye, wangalimwandikia tiimbi la vitabu kuisifu busara yake. Sifa za ujasiri wake kamwe hazingewatoka vinywani mwao!

Hata hivyo, kunatofauti nyingine kubwa kati ya binadamu na hayawani. Tofauti hii inaweza kumvua binadamu sifa zake zote na kuuona ukwasi wa maarifa yake kama ishara ya maangamizi ya ulimwengu. Hii ni kutokana na hasara anayosababisha katika mazingira tulivu waliyoumbiwa viumbe wote.

Uzuri wa ulimwengu tunaoishi humpendeza kila kiumbe hata yule anayemchukiza binadamu kama nzi. Wote hufurahia mazingira yao; hewa safi itokayo milimani, chemichemi, mito na vijito nmamotiririkamaji safi, vilele vya milima vilivyokumbatiwa na theluji daima dahari, yakiwemo mabonde na tambarare zinazohimili uhai wa viumbe wengi.

Urembo huo wa kiasili hauwezi kukamilika bila vichaka na misitu inayoipamba sayari hii huku ikileta mvua. Mapambo yote haya huendeshwa na nguvu za maumbile; nguvu ambazo hazisababishwi na binadamu ingawa sasa yumo mbioni kuzikwamiza kwa kisingizio cha maendeleo. Binadamu anaelekea kuwa hatari kwa uhai wake na ule wa viumbe wenzake kwa sababu anayaharibu maumbile kwa kiasi kikubwa kinachomtisha yeye mwenyewe. Hii ni kwa sababu gani? Sababu zipo nyingi.

Sababu mojawapo ni uchafuzi wa maji kama rasilmali muhimu ya kiasili. Uchnftizi huu umewaletea viumbe na mimea maafa mengi, yakiwemo maradhi mbalimbali. Kwa kweli bila maji, uhai u tatoweka duniani. Uharibifu mkubwa wa



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

maj i husababishwa na binadamu katika harakati zake za kuj iimarisha kimaisha. Kutiririka kwa maji machafu yenye sumu hasa kutoka viwandani na kuingia kwenye mito na bahari huwadhuru viumbe wengine ambao makao yao ni majini. Maji hayo huleta madhara si tu kwa mimea balil hata kwa binadamu kupitia kwa ulaji wa vyakula.

Misitu na rasilmali nyingine inayokimu viumbe lakini binadamu anaiponza. Ukataji wa miti kiholela hasa kwenye sehemu za chemchemi husababisha uhaba wa mvua, Uhaba huo nao huleta kiangazi kinachokausha mimea na visima vya maji. Mchapuko wa ujenzi wa viwanda hasa katika nchi zilizostawi umesababisha uchafuzi wa hewa ambayo pia ni kiungo muhimu kwa viumbe. Uchunguzi uliofanywa na wanasayansi wanaohusika na hali za anga umesababisha taharuki na wasiwasi mwingi. Hii ni kwa sababu umeonyesha kuwa ule utandu unaozuia miale ya jua kupenya moja kwa moja kwenye sayari hii na kuhatarisha uhai, sasa linaanza kutoweka taratibu. Hi ni kutokana na hewa chafu itokayo viwandani. Kwa kadri binadamu anavyozidi kujiimarisha kiviwanda ndivyo ambavyo mabald ya viwanda yanavyozidi kuchafua hewa. Punde si punde, tutakabiliana ana kwa ana na miale mikali ya jua yenye sumu. Ifikapo hatua hii, biandamu atakuwa amechangia pakubwa katika kutowesha uhai wa viumbe wote ulimwenguni!

Mikutano mingi ya kimataifa imefanywa na bado inaendelea kufanywa kila uch ao ili kutahadarisha umma wa ulimwengu dhidi ya uharibifu wa mazingira na mali asili. "Ajenda" za mikutano hiyo hLisa zinalenga nchi zilizostawi kwani hizi ndizo zinazochafua mazingira kwa kasi zaidi kuliko zile zinazostawi. Mapendekezo


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

mengi yametolewa katika vikao hivyo ili kusuluhisha tatizo hili lakini ni hatua chache mno zinazochukuliwa kurekebisha mambo.

Inatupasasisiwenyeweloichukuaju^^ Tuwafunzepiawatotowetukuhifadhi mazingira yao na kuyaweka safi. <u>Tukumbuke kuwa mwana hufuata kisogo cha nina</u>. Mazingira yanapochafuliwa au kuharibiwa, afya zetu zimo hatarini, na hali hii pia ni tisho kwa viumbe wengine, hata vimatu! Kila mmoja wetu anawajibika kutirnza mazingira anamoishi kwa manufaa yetu sote na kwa vizazi vijavyo.

**<u>Maswali</u>**

a) Kulingana na taarifa hii, kwa nini binadamu anahesabiwa kuwa na uharibifu mkubwa kushinda wanyama wengine? (alama4)

b) Onyesha uhusiano uliopo baina ya maendeleo ya binadamu na uharibifu wa mazingira (alama4)

c) Ni kwa nini mwaiidishi anahofia zaidi athari za miale ya jua? (alama 2)

d) Eleza kwa ufupi hasara zinapoweza kusababishwa na uharibifu wa mazingira (alama 5)


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

e) Taja hatua mbili ambazo mwanadamu angeweza kuchukua ili kupunguza madhara ya viwanda. (alama 2)

f) Kulingana na makala haya ni nini maana ya methali, "Mwana hufiiata kisogo cha nina"? (alama 1)

g) Eleza maana ya

i) kusana

ii) mchapuko (alama 2)

# MATUMIZI YA LUGHA

1. (a) ***Andika sifa bainifu za sauti***

(i) e:-

(ii) n:-

(b) ***Eleza maana ya :-***

(i) Kiimbo:.

(ii) Shadda…



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(c) ***Tunga sentensi moja moja kudhihirisha ngeli zifuatazo***:-

(i) U-U

(ii) Pokomo /Pa-ku-mu

(d) ***Unda kitenzi kimoja kutokana na nomino*** '**Mtubia**"

(c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi '***ku***'

(f) Tunga sentensi ya maneno manne ambayo ina sehemu zifuatazo. Kielezi cha namna, kivumishi,kitenzi na jina

(g) ***Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi***:-

Ng'ombe aliyeletwa juzi ameuzwa leo jioni.

(h) ***Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo:-***

(a) Alama ya mshangao

(b) Mshazari

(i) **Tunga sentensi sahihi ukitumia –*wa*- katika kauli ya kutendeana**

(j) ***Andika udogo wa sentensi:-***

Ndama wa ng'ombe yule ameuzwa.

(k) ***Onyesha tofauti ya vitate vifuatavyo kwakukuvitungia sentensi***

(i) Dhamani



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(ii) Thamani

(l) ***Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi***

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari

(m) ***Ainisha shamirisho /yambwa katika sentensi ifuatayo***:-

Mchezaji alimpigia mwenzake mpira kwa mguu wa kushoto.

(n) Huku ukitumia mifano mwafaka, eleza tofauti ya sentensi sahili na ambatano

(o) ***Onyesha aina za viambishi katika sentensi hii***:

Nitajisomea

(p) ***Andika katika usemi wa taarifa:-***

Tutaanza mashindano kesho, Mwalimu alimwambia mwanafunzi.

(q) ***Eleza maana mbili ya sentensi***:-

Tumetengeneza barabara

(e) ***Tumia mifano mwafaka kueleza aina za mofimu***

2. a) Unda nomino za/lm,k, dhahania kutokana na maneno yafuatayo :-

i) Kwea .

ii) Himarisha …



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

b) Huku ukitoa mifano eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili

c) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi: 'umba'

d) Andika katika

Meza ii hii ndiyo aliyotumia kulia

e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa

i) cha …

ii) nywa

f) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:

atakuajiri

g) Sisi tunajua sheria ingawa tu wafisadi

Anza: Japo………….

h) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

i) Wanafunzi wote wameingia darasani

ii) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani

i) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia njia ya matawi** :-

Amekuja kuwatembelea manusura waliopata ajali ya ndege

j) Taja sifa mbalimbali za sauti zifuatazo:



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**/Z/**

**/K/**

k) Huku ukitumia mifano ya sentensi eleza matumizi **mawili** ya kiambishi, **'ji'**

l) **Andika udogo wa:**

Magari yote yaliyobakia yatauzwa na mzee yule mwembamba

m**) Sahihisha:**

i) Kila mwanafunzi alipewa ndazi na mayai moja

ii) Nipee huo mkoba nitoemo vitabu zangu

n) **Tumia – 'ako' katika sentensi kama**:

i) Kivumishi

ii) Kiwakilishi

iii) Kitenzi

o) Bainisha aina **mbili** za vishazi katika sentensi hii :-

Shamba lile kubwa litauzwa kesho

p) **Andika katika usemi wa taarifa** :

"Karibu Rahma, tafadhali kaa," Musa akasema . Ahsante, je, habari za hapa?' Rahma aliuliza

q) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi tofauti ya neno: '**somo'**



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**3.** (a) Taja sauti **mbili** ambazo hutamkwa nyuma ya ulimi kati ya hizi

/h/,/o/,/y/,/u/,/kh/,/g/,

(b) Ng'oa kisiki hiki haraka askari akaamrisha mahabusu

(**Andika kwa msemo halisi**)

(c) **Badili sentensi zifuatazo katika kauli iliyoonyeshwa kwenye mabano**

(i) Si vizuri mwanafunzi kumwibia mwenzake pesa (**Kutendeana**)

(ii) Mpishi aliharibu mchuzi huu kwa kuongeza chumvi nyingi. (**tendeka**)

(d) **Bainisha matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo**:-

Alipowasili alionyeshwa walipo.

(e) **Andika kwa usemi wa taarifa:-**

"Wasichana wakielimishwa wataweza kuwa bora kuliko wavulana," Naibu wa Chansela wa chuo Kikuu aliwaambia mahafala.

(f) **Tunga sentensi ambayo ina aina za maneno uliyopewa:-**

N + V + V + T



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(g) **Tumia ''O'' rejeshi ya kati**

Lisemwalo silo liwalo

(h) 'Msipokuwa wenye bidii hamtayapata mafanikio maishani.' Yakinisha katika umoja

(i) **Changanua kwa kutumia mishale**

'Mimi sikumwona wala Mwenda hakumwona'

(j) **Tunga sentensi ukitumia maneno haya katika kinyume**.:-

(a) afikiana

(b) sifu

(k) **Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo:-**

(i) abudu

(ii) fisidi

(l) **Andika katika hali ya ukubwa**

Mwanamke huyu amezaa watoto wanne.

(m) **Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigwa mstari**

(i) **<u>Mbio</u>** hizi hazitakufikisha mbali

(ii) Mwambie Abedi asifanye **<u>mbio</u>** kuhusu hiyo kazi.

(n) **Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi**



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Msichana aliyeitwa alikuwa mkorofi

(o) **Eleza dhana zinazowakilishwa na viambishi awali katika sentensi zifuatazo: -**

(i) Aliitwa

(ii) Hakupata

(p) **Tunga sentensi mbili kubainisha maana tofauti ya maneno yafuatayo:-**

(i) Kuna

(ii) guna

(q) **Taja mianzo mitatu** tofauti ya ngeli ya **U-ZI**

(r) **Eleza maana ya semi hizi :**

(i) Kunja jamvi

(ii) Piga kambi

**4. Matumizi ya lugha**:

a) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya umoja.

i) Mkitusaidia, nasi tutawanunulia zawadi nzuri. (alama 2)

ii) Waliposikia sauti hizo, waliwarushia mawe hadi wakafa. (alama 2)

b) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

i) Alifuatwa hadi akashikwa na mmeo dukani. (alama 2)

ii) Kuna tofauti gani kati ya sentensi hizi?

Ukirudi tena, nitakuadhibu vilivyo.

Ukirudi, tena nitakuadhibu vilivyo. (alama 2)

c) Sahihisha sentensi hii bila kubadilisha maana.

i) Mkutano ulihairishwa hati ijumaa. (alama 1)

ii) Fuata maagizo uliopewa katika kujibu swali hili.

Wananchi walimpokea mjumbe kwa shangwe na vigelegele. (Tumia.. pokelewa).

(alama 2)

d) Igawe fungutenzi ifuatayo kwa kubainisha kila sehemu huku ukionyesha na kufafanua maana ya visehemu hivyo vinavyounganishwa ili vifanye sentensi kamili. (alama 6)

**Alikiangusha**

e) Tunga sentesi ukitumia maneno yafuatayo ili kudhirisha tofauti ya maana kati yao.

(alama 3)

(i) bovu (iii) bofu

(ii) pofu

f) Chagua neno ambalo haliambatani na mengine.

i) nyerere, ushanga, bangili, shimere. (alama 1)

ii) bunga, punguani, mkatili, baradhuli. (alama 1)

iii) Unganisha sentensi hizi ili ziweze kuwa sentensi moja.

1. Kelvin ni mwadilifu



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

2. Kelvin aliteuliwa kuwa kiongozi. (alama 2)

g) Eleza maana ya misemo hii

i) Shika sikio. (alama 2)

ii) enga enga mtoto. (alama 2)

h) Andika upya sentensi hii kwa kuandika neno lenye maana sawa na lile lililopigwa mstari.

i) Mfalme yule alighadhabika alipofedheheshwa na watumishi wake katika karamu ile. (alama 1)

ii) Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lililopigwa mstari

Wifi alipovaa nguo na kusimama, ajuza yule alikaa. (alama 2)

i) Andika sentensi hii katika hali ya udogo .

i) Mtoto mdogo alipatikana ndani ya nyumba ile. (alama 2)

ii) Eleza maana ya PO kama ilivyotumiwa katika sentensi hizi. (alama 2)

Wanafunzi wachelewapo, huchapwa viboko vinne.

Wanafunzi wanapochelewa, huchapwa viboko vinne.

j) Andika sentensi ifuatayo kwa wakati uliopo.

i) Yusuf hakulima shamba lake. (alama 1)

ii) Andika sentensi hii katika msemo halisi.

Mariam alimshukuru Edith na kutaka kujua wakati aliporudi kutoka nyumbani. (alama2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**5.MATUMIZI YA LUGHA .**

---

A. (a) **Ainisha sentensi hizi** *(alama 4)*

Maji ukiyavulia nguo yaoge

Twende kwetu sasa hivi

(b) **Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi ; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.** ( alama 4 )

(i) Anafanya kazi kwa mwajiri wake .

(ii) Alifanya mambo kisirisiri.

(c) **Toa jibu moja sahihi linalooana na tungo ulizopewa** *(alama 2)*

(i) Mabaki ya jengo lililobomoka au mtu aliyekonda kupita kiasi

(ii) Sehemu ya pwani ambayo meli hufungwa ili kupakia shehena

(d) **Sahihisha sentensi zifuatazo** *(alama 4)*

(i) Uko na pesa yoyote unikopee ili niweze kukidhi mahitaji yangu ?

(ii) Yule msichana anijiringa tu bila kujua kuna kuringa hiyo haitamsaidia sana .

(e) **Taja kinyume cha kila mojawapo ya maneno yafuatayo** *(alama 4)*

(i) Kudai

(ii) Unganisha



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(f) **Unda majina mawili kutokana na kila kitenzi ulichopewa** (*alama 4)*

(i) Tatua

(ii) Kunja

(g) **Eleza maana ya semi hizi** *(alama 4)*

(i) Kata kalima

(ii) Kuzua maneno

(h) **Andika upya sentensi hizi bila kutumia neno amba** *( alama 4)*

(i) Ugonjwa ambao ni hatari sana ni ukimwi .

(ii) Nilimwona simba akinyemelea banda la ng'ombe nilipokuwa nikishika zamu

**Kanusha sentensi hizi** . *( alama 2 )*

(i) Nitaenda bungeni alasiri kuhudhuria kikao .

Tumesimama hapa sana .

(k) **Andika maneno haya katika hali ya kufanyiana** *( alama 2 )*

(i) Soma

(ii) Iba

(l) **Huyu ni nani?** *( alama 1)*

(i) Mwamu

(ii) Kamilisha methali ifuatayo *(alama 1)* .

(iii)Mkataa wengi

______________________________



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

## 6. MATUMIZI YA LUGHA

a) Andika kwa maneno. (alama 2)

(i) 11,001

(ii) 10,001

b) Eleza sifa zinazofananisha na kutofautisha sauti zifuatazo. b na d.
(alama 3)

c) Eleza matumizi ya viambishi VITATU vya ngeli ya MAHALI huku ukivitungia sentensi mwafaka.
(alama 3)

(d) **Tunga sentensi ukitumia neno 'kuja' kama:** (alama 2)

(i) Nomino

(ii) Kitenzi

(e) **Tunga sentensi ukitumia vielezi vinavyotokana na maneno uliyopewa.**(alama 3)

(i) Soko

(ii) Zidisha

(iii) Mtoto

(f) **Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.** (alama 3)

Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(g) **Tunga sentensi sahili yenye viungo vya sarufi vifuatavyo.**

(alama 3)

(i) Shina la kitenzi cha silabi moja

(ii) Kauli ya kufanyia

(iii) Kikanushi

(iv) wakati uliopita

(v) Mtendewa nafsi ya tatu umoja

(vi) Kiima nafsi ya pili wingi.

h) Neno 'tikiti' hupatikana katika NGELI mbili tofauti. Taja NGELI hizo huku ukitunga sentensi mbili kubainisha matumizi tofauti. (alama 3)

(i) **Tunga sentensi sahihi ukitumia viunganishi vyenye dhana ya:**

(i) Kinyume (alama 2)

(ii) Kutowezekana kuwili.

(j) **Andika kwa wakati ujao** (alama 2)

Ungalifanya kazi kwa bidii usingaliishi maisha ya dhiki.

(k) **Tumia neno 'mpaka' kama kihusishi cha:** (alama 3)

(i) Kiwango

(ii) wakati

(iii) Mahali

(l) **Kamilisha sentensi kwa kutumia vivumishi kama ulivyoagizwa.**

(alama 3)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(i) Rehema ni bibi …………………………… bezo . (umilikaji)

(ii) Naomba kinywaji …………………………… (ziada)

(iii) Muonye bawabu …………………………….. kwa kutofika mapema. (kusisitiza- mbali kidogo)

(m) **Tofautisha kimaana** (alama 2)

(i) Aliuawa mnyama.

(ii) Mnyama aliuliwa

n) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi tofautiya ‘po’. (alama 2)

o) Andika kwa msemo halisi. (alama 2)

Askari alisema angemuona siku hiyo jioni dukanimwe.

p) Tunga sentensi ukitumia ulivyopewa katika kauli ya kutendewa. (alama 2)

(i) Pa

(ii) La

**7.MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli zipi**?**

i) neno ……………………………….

ii) mate ………………………………. (alama 2)

(b) Eleza matumizi mbalimbali ya ‘ni’ katika sentensi ifuatayo. (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani

(c) Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo

i)/dh/ ……………………………………

ii)/gh/ …………………………………….. (alama 2)

(d) Ainisha matumizi ya –ema katika sentensi ifuatayo (alama 3)

Mwanafunzi mwema ametunzwa vyema kwa wema wake

(e)Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)

"Atamkuta papa hapa akija kesho".Alisema.

(f) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(g) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Tano ondoa tatu matokeo ni mbili (anza: Mbili…………) (alama 1)

ii) Mwalimu huyu anafunza Kiswahili



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(Maliza kwa kiashiria kisisitizi) (alama 1)

iii)Ng'ombe aliyekuwa nyuma ya ua alichechemea kwa vile aliumia ukwato wake. (andika kwa wingi)
(alama 2)

(h) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno lifuatalo (alama 2)
Ndwele

(i) Ainisha sentensi hii [alama 3)
Aliyenichokoza
(j) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli ya kutendewa (alama 4)
i) Muktubi amempa mwanafunzi jarida.

ii) Bate alivua samaki wengi.

(k) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo
(alama 4)
i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

ii) Kuonyesha chanzo

(l) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari/vishale (alama 4)


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kandanda ni mchezo maarufu duniani

(m)Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Wanafunzi ambao waliokuwa wakarimu walimpenda Bi Keti

(n) Yakinisha sentensi hizi (alama 2)

i) Asingeenda safari asingepata ajali

ii)Usije

o) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezewa mawanjani

**8.**

(a) Bainisha aina ya vivumishi katika sentensi hii

Nyumba yangu ina maridadi

(b) Kamilisha jedwali

| | | |
|---|---|---|
| Kufanya | kufanyia | kufanywa |
| Kula | _____ | |
| Kuunga | ______ | ______ |



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(c) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi hii

Aliimba kwa sauti tamu

(d) Andika kwa wingi

Pahala hapa ni pake

(e) Eleza mtumizi ya na katika sentensi:

Halima na Asha wanasaidiana

(f) Huku ukitoa mifano, fafanua miundo mitatu ya majina katika ngeli ya LI-YA

(g) Onyesha (i) Kielezi (ii) Kitenzi katika sentensi: Mvua ilinyeshamfululizo

(h) Kanusha sentensi hii:

Tumechukua nguo chache kuuza

(i) Tumia-ndi-pamojanaviashiria vyangelikujazamapengo cw-

(i) Wewe _____ninayekutafiita

(ii) Nyinyi______mnaoongoza



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(j) Andika sentensi hiiupya kwa kufuatamaagizo

(i) Nilikuwa nimejitayarisha vizuri kwa hivyo sikuona ugumu wowote katika safari yangu

Anza: Safari............ (alama2)

(k) Geuza vitenzi hivi viwe majina

(i) Shukuru

(ii) Enda

(1) Eleza maana mbili tofauti za sentensi hii. Mamake Juma na Mariamu walitutembelea

**9.**

a) Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya I -1

b) Changanua sentensi ifiiatayoukitumiamchoro wa matawi: Mkulima mzembe amepata hasara

c) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimchezea

d) Taja sauti mbili zinazo tamki wa midomoni



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

e) Kanusha sentensi ifiiatayo: Ningaiikuwa napesa ningalinunua nyumba.

f) Kitenzi Fumbata kiko katika hali( kauli) ya Tendata, Fanyata.

g) Tunga sentensi ukitumiakielelezi cha:

i) Wakati ii) Mahali

h) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Mhunzi mrefu alisliinda tuzo (anza kwa: Tuzo.....) ii) Mwanaftinzi huyu anasoma Idf aransa (Anza kwa Idashiria kisisitizi)

i) Sentensi hizi ni za aina gani?

i) Lonare anatembea kwa kasi.

ii) HalimaanaandikahaliEkomwa anasoma.

j) Tunga sentensi moja ukitumia neneo "seuze"

k) Bmnisha kirai nomino na Kirai Tenzi katika sentensi:

Jirani mwema alinipa chakula)

l) Unda Nimino kutqkana na vitenzi

i) Chelewa ii) Andika



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

m) Onyesha hali katika sentensi zifuatazo:

i) Huenda mvua ikanyesha leo.

ii) Miti hukatwa kila siku duniani

n) Unganisha sentensi zifuatazo ukitumianeno "japo"

i) Selinaalijitahidi sana ii) Selinahakushindambiohizo.

o) Andikakinyumecha: - Mwise alikunja nguo aliokua ameanika.

p) Sahihisha sentensi:

q) Andlka katika msemo wa taarifa. "Sitathubutu kumpa pesa zaagu" Mkolwe alisema.

r) Tunga sentensi kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo:

Suka na Zuka

s) Eleza matumizi ya ritifaa katika: N'shamchukua

t) Andika udogo na ukubwa wa neno'kiti'

u) Eleza matumizi ya "na" Katika sentensi:

Sofia na Raeli wanaandaliwa chai na mpishi

**10.**



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

a) Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania.

b) Eleza maana mbili za sentensi ifoatayo:

Hawa ni watoto wa amarehemu Bwana Nzovu na Bi Makamo. (alama 2)

c) Unda nomino moja kutokana na kitensi "ghafilika". (alama 1)

d) Andika kwa wingi:Nyundo hii imevunjika mpini wake.
(alama 1)

e) Ainisha sentensi ifuatayo ukitumiajedwali. (alama 3)

Mvulana mrefu anavuka barabara

f) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi ziftiatazo:

i) Mtoto mwenyewe alienda shambani. (alama 1) ii) Kazi yetu haihitajiki shuleni. (alama 1)

g) Koloni/nuktambili(:)hutumiwa katika kuorodhesha. Onyesha matumizi mengine matatuyakoloni(:) (alama 3)

h) Tunga sentensi itakayoonyesha matumizi ya kihusishi cha a-unganifu. (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

i) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika seiatensi ifuatayo 'Mkulima

aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri (alama 2)

j) Ainisha viambishi katika neno: kujidhiki. (alama 2)

k) Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo

'Kalamu aliyokuwa nayo Mwalimu ni ya mwanafunzi. (alama 2)

l) Andika viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo:

i) Chakula...............................................................

(alama 1)

ii) Kwetu.

m) Badilisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali ya kuamuru. Baba ingia ndani. (alama 2)

n) Elezamaanaya sentensi

'Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyurnba na ningalistarehe'. (alama 2)

o) Fafanua aina za hali zinazotumika katika sentensi hizi.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

i) Mwimbaji aliimba, akacheza na akachanganisha sana. (alama 1)

ii) Shangazihujakilamara. (alama 1)

p) Andika. Katika mnsemo wa taarifa ‘nitakuarifu nimkimwona’, Elma alisema. (alama 3)

q) Nyambua kitenzi "ota" kama kinavyotokea katika kirai "ota ndoto" ili tofauti tatu zilitoke (alama 3)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**11.**

a) Tambuamzizi katika neno. (alama 1)

“msahaulifu”.................

b) Tunga sentensi ukitumiakivumishichanomino. (alama 1)

c) Andikakinyumecha:

Wasichanawatatuwanaingiadarasanikwaharaka (alama 2)

d) (i) Fafanua maana ya “mofimu huru” (alama 1)

(ii) Toa mfano mmoja wa mofimu huru.

e) Tambua kiambushi awali na tamati katika neno alaye. (alama 2)

Tumia kirejeshi-amba-kuunganisha sentensi ziluatazo:

(i) Mwanafunziwlenimrefli.

(ii) Mwanafiinziyuleamepitaintihani. (alama 2)

g) Sahihisha sentensi hii:

Waya yangu imepotea ................... (alama 1)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

h) Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:

Mpishi amempikia mgeni wall vizuri. (alama 1)

i) Ibadilishe chagizo ya mbahali kwa vile ile ya wakati katika sentensi ifuatayo:

Mchezaji aliucheza mpira mjini Malindi.

j) Elezamaanambiliza sentensi:

Yohana alimpigia Husha mpira,

Yohana alipiga mpira badalayaHusha

k) ' Kanusha:

Sisi tumemaliza kujenga nyumba ambayo ingaikuwa yake angalifurahi

................................................................. (alama 1)

l) Undano minokutokanana

i) Zingua...................................................................... (alama 1)

ii) Tosa.................................................................... (alama 1)

m) Ichoree vielezo matawi sentensi:



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Paka mdogo amepanda mchungwani. (alama 2)

n) Tumia **kihusishi badalia** kutunga upya sentensi hii:

Mgeni yuko katika nyumba (alama 2)

o) Undakitenzikutokanananen “sahili”

........................................................... (alama 1)

p) Eleza tofauti kati ya sauti (z) na (d) (alama 2)

q) Tambua aina ya kitenzi kilichopigiwa mstari katika sentensi. Mzee huenda anacheza kamari. (alama 1)

r) Badilisha kiwakilishi kimildlishi kwa kiwakilishi kionyeshi katika sentensi:

Cha keki lipatikanao chini (alama 1)

s) Tumia mfano mmoja mmoja kutofautisha baina ya **sahili** na **ambatano**. (alama 4)

(t) Tunga Sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha nomino (alama 1)

(u) Andika kwa wingi:



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Mvu imebomoa nyumba ya jirani

v) Akifisha kifungu kifuatacho:

huenda serikali iwezie kuidhibiti bei ya petroli hatuwezi kuyaruhusu makampuni ya petroli kuuyanyasa umma alisema waziri wa kawi bei ya petroli imeongezwa maranne katika kipindi cha mwezi mmoja.

# ISIMUJAMII

1. Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa kiswahili nchini Kenya

2. (a) Ni mambo yapi yanayochangia kudidimia kwa Kiswahili nchini Kenya.

   (b) Mambo haya yanaweza tatuliwa vipi?

3. a) Bainisha kwa kutoa mifano sifa **tano** za lugha ya vijana '**sheng'**

   b) Fafanua changamoto **tano** zinazozuia maenezi ya haraka ya lugha ya Kiswahili

4.

(a) Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. (alama 2)

(b) Taja mambo mawili yanayoonyesha udhaifu katika mazungumzo na huchangia katika uhamishaji wa msimbo. (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

c) Taja kaida mbili zinazotawala matumizi ya maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka.

(alama 2)

d) Fananisha sifa zozote nne za sajili za maabadini na mahakamani.

(alama 4)

**5. ISIMU JAMII**

"Bwana mdogo," alisema kwa sauti ya kite.

'Naam Doctor,' Nikajibu.

'Leo wasikiaje?'

'Nafeel poa'

'Unafanya kazi gani?'

'Nasukuma rukwama'

'Eeh! Bwana, kama watakwa kuishi,acha hiyo kazi ya suruba, unasikia?'

'Ndiyo Doctor"(kisha akanipimapima kwa kifaa alichokuwa nacho…..)

'Leo!' Aliniambia huku akisimama wima na kuchezeshachezesha kifaa chake mkononi,

"N'takuruhusu kwenda nyumbani.Wapaswa kupumzika kwa mwezi mzima pasi kufanya lolote zito."

'N`takupa vidonge vya kumeza.'

'Asante Doctor ,' Nikamshukuru.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**Maswali**

a) Mazungumzo haya yako katika rigista gani? (alama 1)

b) Taja lugha zilizotumika katika mazungumzo haya (alama 2)

c) Fafanua sifa za sajili hii (alama 3)

d) Eleza dhima za lugha ya Taifa (alama 2)

e)Taja na ueleze matatizo mawili yanayoikumba lugha ya Kiswahili. (alama 2)

**6.**

*Soma kifungu kifutacho kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Kwa mujibu wa sheria kifungu nambari 3 sehemu ya A ya sheria za nchi, umepatikana na hatia ya kutatiza utulivu wa raia wapenda amani kwa kuwatusi na kutisha kuwapiga. Kiongozi wa mashtaka amethibitisha haya kwa kuwaleta mashahidi ambao wametoa ushahidi usiotetereka kuhusu vitendo vyako katika tukio hilo. Korti hii imeonelea una hatia na imeamuru ufungwe jela kwa muda wa miaka miwili bila faini ili liwe funzo kwako na kwa wenzako wenye tabia kama zako. Una majuma mawili kukata rufani.

**(alamal)**



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

b)Toa ushahidi wajibu lako (alama3)

c) Zaidi ya sifa zilizo katika kifongu hiki, Eleza sifa zingine sita za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (alama6)

**7**

a) Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua kaida tano katikajamii ambazo matumizi ya

lugha hutegemea. (alama 10)

**8.**

a) Eleza huku ukiota mifano sifa tano za kimsingi zinazo tambulisha sajili ya mazungumzo. (alama 10)

# USHAIRI

1. 1. Nitampa nani, sauti yangu ya dhati
Kwa kipimo gani, ingawa kiwakatiti
Amefanya nini, la kutetea umati
Kipimo ni kipi?



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

2. Yupi wa maani, asosita katikati
Alo na maoni, yasojua gatigati
Atazame chini, kwa kile ule wakati
Kipimo ni kipi?

3. Alo mzalendo, atambuaye shuruti
Asiye mafundo, asojua mangiriti
Anoshika pendo, hata katika mauti
Kipimo ni kipi?

4. Kipimo ni kipi, changu mimi kudhibiti
Utu uko wapi, ni wapi unapoketi
Nje kwa mkwapi, au ndani kwa buheti
Kipimo ni kipi?

**Maswali**

a) Eleza umbo la shairi hili

b) Taja na ueleze jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wa ushairi

c) Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi

d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha ya nathari


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

e) Taja bahari **tatu** zinazojitokeza katika shairi na utoe sababu

f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi hili

i) Katiti

ii) Gatigati

iii) Mangiriti

2. **KIPI NIKITENDE?**

. Tayari ni sarakani, niambie yote johara,
Mosi nimpe shukrani, kanizaa bira zira,
Wapo haiko hisani, ningefaa kwa uparara**,**
Kipi takachokitenda, ni nene heko kwa mama?

. Miezi tisa tumboni, yote nina kajinyima,
Kanikopa uchunguni, safari ndefu kazima'
Kama kinda kiotani, kiniasa huyu mama'
Kipi takachokitenda, ninene heko mama ?

. Baba siku jana madadi, **kawa vingaito mambo,**
Kaolewa na asadi, kachalazwa kwa **wimbombo**,
Kaona – bali jadili, kuchao puani bombo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

.
Kila kuchao zarani, kupalilia kondeni,
Kachanika mpinini, chungu povuka motoni,
Kaviyariya fingani, kinijali jikoni,
Kipi tukachokitenda , ninene heko mama?

.
Wa siku hizi vijana, wakahujuru nyumbani,
Wengine wao jagina, kawa lofa mutaani,
Hali ukashiba nina, afikapo tu, "**kongoni!"**
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

.
Nawe bwana siwe maya, vita hasha kiwa kombo,
Tena simfanye yaya, ya kikoa ndio mambo,
Simtende ya hizaya, siwe mwao kila jambo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

.
Sasa jamvi nakuja, kisa nimesakarika,
Naomba niliyotaja, tatia manani kaka,
Nenayo yasiwe ngoja, ili nipokee baraka,
Mema nitamtendea, apate futahi pia.

**Maswali**

(a) Eleza umbo la shairi hili

(b) Kwa nini msanii amshukuru mamaye ?


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(c) Ni kina nani wanaokashifiwa na msanii ? Kwa nini ?

(d) Onyesha tofauti katika ujumbe iliyoko katika beti nne za kwanza na mbili zinazofuata

(e) Toa majina mengine yenye maana sawa na haya yaliyotumiwa katika shairi hili :

(i) Mama

(ii) Dawati

(iii) Imara/thabiti

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kaika shairi:

(i) Kawa vangaito mambo

(ii) Wimbombo

(iii) Kongoni

3. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

**<u>MWANAMKE</u>**

1. Namwona yu shambani,
Na jembe mkononi,
Analima,
Mwanamama,
Mavuno si yake,
Ni ya mume wake.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

2. Namwona viwandani,
Pia maofisini,
Yu kazini,
Hamkani,
Anabaguliwa,
Na anaonewa.

3. Namwona yu nyumbnai,
Mpishi wa jikoni,
Yaya yeye,
Dobi yeye,
Hakuna malipo,
Likizo haipo.

4. Namwona kitandani,
Yu uchi **maungoni.**
Ni mrembo
Kama chombo,
Chenye ushawishi,
**Mzima utashi.**

5. Namwona mkekani,
Yuwamo uzazini,
Apumua,
Augua,


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kilio cha kite,
Cha mpiga pute.

6. Kwa nini mwanamke,
Ni  yeye peke yake,
Heshimaye,
Haki anakosa,
**Kwa kweli ni kosa**

***(Muhammed Seif Khatib)***

.(a) "**Shairi hili ni la kukatisha tamaa**". Fafanua dai hili kwa kutoa mifano **minne**

(b) Eleza umbo la shairi hili

(c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari

(d) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima utoe mifano **miwili** ya jinsi ilivyotumika

(e) Onyesha mifano miwili ya ubabadume inayojitokeza katika shairi hili

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi:

(i) mzima utashi

(ii) maungoni

4. **KIACHE KINACHONG'AA**

Katu siwe na harara, wala moyo kukupapa,
Usichukue hasira, na moyo kutapa-tapa,
Utaharibu na sura, mwishowe uende kapa,


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Mbeleye kina madhara, kile kinachokukukwepa,
Mbele yake ni hasara, si chema kitakutupa,
Hutaipata ijara, kuchuma ama kukopa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Hicho jangwa la Sahara, si mnofu ni mfupa,
Hakina njema ishara, humtupa mwenye pupa,
Kibovu kama tambara, hupasuka kama chupa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Kitaleta ufukura, si huko wala si hapa,
Kina mengi mazingira, na mbele kitakuchapa,
Sijitie usogora, ukavimbisha mishipa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Si kazi yenye ujira, mshahara kukulipa,
Ya cheo chenye kinara, na heshima wakikupa,
Mbele haina imara, japo leo wajitapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Japo kazi ya biashara, kutwa wauza makopa,
Uwe mtu na kipara, Mwananchi ama Yuripa,


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Bora uwe na busara, fedha tajaza mapipa,
    Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara
Usione kinang'ara, huku chapiga marapa,
Ukimbilie kupora, moyo wako kukuzipa,
Kitakugeuza chura, mbele yake utaapa,
    Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Usitupe sarara, nyuma kisogo kuipa,
Ukaenda kwa papara, kiumbe mbele kitanepa,
Kwanza tumia fikira, uchague njema chapa,
    Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Na sisemi masihara, hakika kweli nawapa
Mlio pwani na bara, wa Mufindi na wa lupa
Maneno haya kitara, muarifu na Wachepa,
    Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Tamati niliyochora, ya shikeni si kuepa
Kisha muwe na basira, na Mola kumuogopa,
Kinachokwepa si nyara, ufunge ndani ya kwapa,
    Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

(a) Eleza hii ni bahari gani ya shairi


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(b) Eleza dhamira ya mshairi

(c) Fafanua hasara nne zinazoletwa na tamaa - vile ving'aavyo

(d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi

(e) Andika ubeti wa tano katika lugha ya nathari

(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi

(i) Kuchuma

(ii) Kisogo kuipa

**5.USHAIRI**

1. Siku moja itafika, nijifungie safari;
   Safari ndefu hakika, isiyotaka magari;
   Magari hayatafika, wala meli za fahari;
   Siku yangu!

2. Siyo nadhiri naweka, katu siyo ubashiri;
   Ni mwendo uliopangika, ni muhali kughairi;
   Kwenda nawajibika, kubeta sina hiari;
   Siku yangu!



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

3. Roho inanitutika, kila nikitafakari;
Ziara is'o shirika, hata akhi hujibari;
Wanabaki kuteseka, na kunipami kwaheri;
Siku yangu!

4. Siku itakapofika, zamani za kuabiri;
Kutazuka hekaheka, kibuhuti cha Suduri;
Na mwingi mno wahaka, kwa wendani na wambari;
Siku yangu!

5. Ziara itafanyika, na mola ndiye Sayari;
Ngia itanimulika, nifike pasi usiri;
Niwache mkitamka, mabayangu na mazuri;
Siku yangu!

6. Binadamu hutoweka, siku yake ikijiri;
Ugeni una mipaka, nami leo nahajiri;
Mipaka yangu yafika, mungu amenihitaji;
Siku yangu!

7. Sina budi kuitika, wito huu wa kahari;
Ziara kukamilika, moyoni sifanyi ari;
Nenda zangu haraka, moyoni sifanyi ari;
Siku yangu!


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

8. Haki sasa naondoka, ni mja sina hiari;
Huko nitasetirika, dahari hata dahari;
Buriani wahibaki, na maswahaba kwaheri;
Siku yangu!

***Maswali:***

a) Mtunzi wa shairi alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili? (alama 3)

b) Idhini ya ushairi/ mtunzi inajitokezaje katika shairi hili? (alama 4)

c) Kwa kutumia ithibati kemkem (kutoka katika shairi hili), eleza kwa undani muundo wa shairi hili. (alama 4)

d) Eleza ujumbe unaotolewa na mwandishi katika ubeti wa saba na nane. (alama 4)

e) Mafungu yafuatayo yametumiwa kumaanisha nini?

i) ni muhali kughairi. (alama 1)

ii) ziara is'o shirika. (alama 1)

f) Toa mifano miwili ya jazanda katika utunzi huu. (alama 3)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

6. Mtu na awe na macho, kamili yote mawili,
Na kila kitu ambacho, alikiumba Jalali,
Kama hana kichwa kwacho, si mtu bali tumbili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Wa kila kitu mwilini, ni yeye huwa wakili,
Na yeye ndiye mashini, ya kuendesha kauli'
Kito cha matumaini, usukani wa akili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Wakili wa kila kitu, viungo vyote vya mwili,
Kichwa kinaleta utu, kwa sifa ya taamuli,
Ama ufanywe utu, kwa sifa ya taamuli,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Mtu huwa ni sanamu, hajaumbika kamili,
Kama hanayo fahamu, fahamu yake thakili,
Si kichwa cha binadamu, binadamu wa asili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Tazama mwendawazimu, kichwa kilotanakali,
Huingiwa na zahamu, kukiuka ya awali,
Mfano wa marehemu, kila kiungo hajali,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kichwa chenyewe si hoja, hoja ubongo mkali,
Kiwe kijua vioja, kwa kamili atikali,
Si kichwa chenye kuvuja, si kichwa chenye manzili,
  Kichwa ni yeye wakali, wa kila kitu mwilini.

Kichwa kiwe peke, juu ya kiwiliwili,
Shingoni ukitungike, na nywele kama ulimi,
Moyo visiunganike, kichwa hakitahimili,
  Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

***Maswali:***

a) Fafanua ujumbe unaobebwa na kiitikio cha utungo huu. (alama 3)

b) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)

c) Mja asiye na 'kichwa' amefananishwa na nini? Toa mifano miwili. (alama 2)

d) Ingawa kichwa ni muhimu, ni sharti kishirikishwe na viungo vipi ili kipate ukamilifu wake? (alama 3)

e) Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu. (alama 2)

f) Eleza mpangilio wa vina katika ubeti wa pili. (alama 2)

g) Taja na ueleze maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi.

i) Neno la mwisho katika utao wa mleo ubeti wa kwanza. (alama 2)

ii) Neno la mwisho katika ukwapi wa mwanzo ubeti wa tano. (alama 2)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

***7.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Wataalamu muwe macho, vuani moto muenge,
Muenge hicho ambacho, cha watu wenye mawenge,
Mawenge yenye kijicho, kiswahili wakivunge,
Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

Sichafue kiswahili, barakala tuwapinge,
Apige kila hali, wasiguse tuwainge,
Tuwainge wende mbali, kiswahili tujijenge,
Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

Sichafue yetu lugha, waharibu Wabanange,
Wabanange iwe nyagha, waiweke tengetenge,
Lugha kuitwa; ulugha, lafidhi watia denge,
Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

Tuichange heshima, na ulugha tuupinge,
Tuhifadhi kwa salama, na kisingio unyonge,
Kelele za maamuna, si watu ni visinge,
Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

Kasema sheikh Amri, kiswahili tukisenge,
Kistawi kinawiri, kitumike kwenye bunge,
Hii ni yetu fahari, lugha yetu tuichunge.


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

Kikipatwa na maradhi, kwa sindano tukidunge,
Kila jama kutidhi, kipatwe hapo tupunge,
Tukitia mfawadhi, kama kunde na kihenge,
Barakala tuwapinge, sichafue kiswahili.

**MASWALI**

(a) Ni mtindo gani aliotumia mshairi katika kutunga ubeti wa 1 na 2. (fafanua kwa kutoa mfano)

(alama 4)

(b) Mshairi ametoa mapendekezo kadha katika shairi kuhusu jinsi ya kuimarisha na kuhifadhi lugha ya kiswahili. Taja na ufafanue matano kati ya hayo. (alama 5)

(c) Mshairi anazungumza na akina nani? Anazungumzia nini? (alama 4)

(d) Mshairi ametumia tamathali mbalimbali kuwasilisha ujumbe wake. Taja mifano mitatu tofauti ya tamathali hizo. (alama 3)

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 4)

(i) Muenge
(ii) Barakala
(iii) Mtawadhi
(iv) Maamuma.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

8. i) Una moyo gani N'nakuuliza Wangu mhisani
Na kiasi gani Unavyojiweza Ijapo tufani
Ukiwa laini Utajipoteza Usijibani
Kusimama Pweke Kwataka Makini

ii) Zitavuma pepo Zitapupuliza Uanguke chini
Ela uwe papo Unajikweleza Na kujiamini
Utikiishapo Umejiuiza Pigo la moyoni
Kusimama Pweke Kwataka Makini

iii) Utie migati Ya kutuoteza Hapo aridhini
Kwa nia na dhati Usiogeuza Au kuihini
Zidate baruti Uwe wapuuza Welele usoni
Kusimama Pweke Kwataka Makini

iv) Sishike vishindo Na mauzauza Ya kukuzaini
Kita kama nyundo Ukinuiliza Unayoamini
Na uje mkondo Utadikimiza Kujipa mizani
Kusimama Pweke Kwataka Makini

v) Wengine wasiwe Unaoweleza Yaliyo maani
Wewe ndiwe Unaoweleza Yaliyo maani
Ela kichukuwe Pia kujikaza Katika midani


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Kusimama Pweke Kwataka Makini

a) Lipe kichwa shairi hili (al 2)

b) Kwa nini kusimama pweke "kwataka makini'' (al 2)

c) Ni hatua gani zinazopendekezwa mtu anayenuia kusimama pweke? (al 5)

d) Andika arudhi za shairi hili (al 5)

e) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi hili (al 6)

i) Muhisani

ii) Migati

iii) Vishindo

iv) Kweleza

v) Mizani

9.Soma shairi lifuatalo na kisha ujibu maswali yafuatayo.

**UKUBWA JAA**

Dunia yetu dunia, watu wanakufitini,
Dunia huna udhia, watu wanakulaani,
Dunia huna hatia, wabebeshwa kila zani,
Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia umenyamaza, umetua kwa makini,
Dunia vitu mejaza, watu wanataka nini?



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Dunia wanakucheza,binadamu maluuni,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia mtu akose, hukutia mdomoni,

Dunia hebu waase, hao watu mafatani,

Dunia chuki mpuse, muipate afueni,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia una lawama, za uongo si yakini,

Dunia wanokusema, ni manjunju si razini,

Dunia huna hasama, waja ndio kisirani,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia kuharibika, hayo amezusha nani?

Dunia watu humaka, hao wanokuhini,

Dunia umejazika, kila tunu ya thamani,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia unatukisha, bwerere bila undani,

Dunia unatukosha, maji tele baharini,

Dunia unaotehsa, mimea tosha shambani,

Dunia unaonewa, umetenda kosa gani!

Dunia hujageuka, tangu umbwe na manani

Dunia watu ndo, nyoka, mahaini na wahuni


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Dunia una baraka, mwenye pupa hazioni

Dunia huna ubaya, wabaya ni insani.

**Maswali:**

(a) Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu yako. (alama 3)

(b) (i) Kichwa cha shairi hili kinaoanaje na maudhui ya shairi?. (alama 2)

(ii) Andika methali moja inayoeleza maudhui ya shairi hili. (alama 3)

(c)Eleza sifa tatu za wanadamu kama anavyoeleza mshairi. (alama 3)

(d)Kwa kutoa mifano kutokana na shairi hili, eleza mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 6)

(e) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo vya maneno kama vilivyotumika katika shairi.

(i) bwerere bila undani

(ii) hao watu mafatani

(iii) afueni

(iv) insani (alama 4)



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

**10. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa....... Tumekataa! Tumekataa


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Hii awamu ya ’Haki ya mtoto wa kike’

**Maswali**

a) Taja mambo matatu muhimu yaliyozungumzwa na mshairi kisha ueleze kila moja. (Alama 6)

b) Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)

c) Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi kisha ueleze kila moja (Alama 4)

d) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni ’awamu’ nyingine?(Alama 3)

e) **Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi** (alama 3)

(i) awamu

(ii) kudhalilishwa

(iii) Dhiki

***11.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo***

1. Mkata ni mkatika, harithi hatoridhiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

2. Sina ngo’mbe sina mbuzi, sina konde sina buwa
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
Mrithi nini wanangu?



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

3. Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi, mno nikukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

4. Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno mi kulaumiwa
Poleni wangu sana, sana kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina , sana la kuacha kuraduwa
Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa
N'nawana na miliki, hadi nitakapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

7. Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongowa
Muwane kwa nyinyi mbinu, mwende pasi kupumuwa
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa
Mrithi nini wananngu?


Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

(a) **Taja** mambo yoyote mawili ambayo mtunzi angewarithisha wanawe. (alama 2)

(b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe. (alama 3)

(c) **Andika** ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)

(d) **Dondoa** mifano miwili miwili ya : (alama 2)

(i) Inkisari

(ii) Tabdila

(e) **Chambua** shairi hili kwa upande wa :

(i) Dhamira (alama 2)

(ii) Muundo (alama 4)

(f) **Eleza maana** ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

(i) Mlimwengu kanipoka

(ii) Sina konde sina buwa.

(iii) Wingi wa shakawa.



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

# FASIHI SIMULIZI

**1.** ***Soma wimbo/shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***

**MUITALIA ANAZWE**

Saa kumi alfajiri
Sote tuliamshwa
Safari tuliianza
Lazima tuimalize
Maji ukiyavulia nguo
Lazima uyaoge

Wazee kwa vijana waliimba
Muitalia lazima anazwe
Mashamba yao walilia
Uui! Jikaze wavulana
Hawataki rangi hii

Wengi wanauliza
Mwitalia alikuja lini? Na ataondoka lini?
Mnaze huyu mlowezi
Hatuchoki
Hatuchoki
Lazima yeye anazwe

Vifaranga na mbuzi



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

Mbavu zao zahesabika

Meee! Sauti zilihinikiza kote

Haya yote hakika, ni madhila ya Muitalia

Nguvu kweli tunayo

Simama mbele tunayo

Simama mbele uone !

Muitalia ondoka !

Au nikuondoe kwa nguvu

**Maswali**

(a) Taja madhila yaliyosababishwa na Muitalia katika makala haya.

(b) Thibitisha kuwa utungo huu ni wimbo.

(c) Eleza maana inayojitokeza katika mistari ifuatayo:-

(i) Mbavu zao zahesabika.

(ii) Haya yote hakika, ni madhilia ya Muitalia.

(d) Huu ni wimbo wa aina gain? Eleza ukitoa ushahidi

(e) Eleza kwa sentensi mbili au tatu shughuli muhimu za kiuchumi za watu wanaimba wimbo huu

(f) Taja mbinu za lugha zilizotumiwa katika wimbo huu. Toa ushahidi

(g) Taja mafunzo mawili yanayotokana na wimbo huu



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes

2. (a) Eleza maana ya miviga kisha uonyeshe inakotumika

(b) Eleza sifa za miviga

(c) Onyesha umuhimu wa miviga

3. Ni nini maana ya wimbo ?

Ni nini maana ya nyimbo zifuatazo.

Tenzi

Kongozi

Sifo

Wawe

Tendi

(iv) Eleza umuhimu wa nyimbo

(b) Eleza sifa za wimbo wa aina ya Bembelezi



Prefer Calling Sir Obiero Amos @ 0706 851 439 for the Marking Schemes


PREFER CALLING SIR OBIERO AMOS @
0706 851 439
FOR QUICK SERVICE
ACQUIRE THE FOLLOWING
KASNEB NOTES/REVISION KITS
NOW :
CPA
ATD
CS
CICT
CIFA
0706851439
By Sir Obiero Amos Resources
&
AMOBI SOFT COPY PUBLISHERS
Transparency, Honesty and Accountability Defined
KASNEB
Study Materials
ATD LEVEL 3 STUDY TEXT
PRINCIPLES OF ECONOMICS
CPA SECTION 4 STUDY TEXT
CIFA SECTION 1 STUDY TEXT
FINANCIAL MATHEMATICS
CS SECTION 6 STUDY TEXT